JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**6 Februari 2026**

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Benki Kuu ya Tanzania itauza kwa njia ya mnada wa hadhara vifaa chakavu yakiwemo magari, pikipiki, mitambo, vifaa vya ofisi, vifaa vya tehama na vifaa vingine katika ofisi zake zilizopo mikoa ya **Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Mtwara** na **Mjini Magharibi (Unguja)**.

Maelezo zaidi ya vifaa hivyo ni kama yanavyoonekana hapa chini.

| Na. | Mkoa | Kituo | Kifaa | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mbeya | Benki Kuu ya Tanzania, Barabara ya Mahakama, S.L.P 1203, Mbeya. | • Samani za ofisi<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa vya tehama<br>• Vifaa vingine | 18 Februari, 2026 |
| 2. | Mtwara | Benki Kuu ya Tanzania, Barabara ya Makonde, S.L.P 1446, Mtwara. | • Samani za ofisi<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa vya tehama<br>• Vifaa vingine | 18 Februari, 2026 |
| 3. | Dar es Salaam | Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884, S.L.P 2939, Dar es Salaam.<br>na<br>Nyumba iliyopo Kiwanja Na. 447, Makutano ya Chole Rd na Lincolin St, (*baadhi ya magari, pikipiki na mitambo*) | • Magari (Toyota Landcruiser, Toyota Coaster, Toyota RAV4, Toyota Hiace, Suzuki Jimmy, Suzuki Grand Vitara, Suzuki Maruti Omni, Nissan Civilian Bus, Mercedes Benz Saloon na Isuzu NPR)<br>• Mitambo (Forklift)<br>• Samani za ofisi<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa vya tehama<br>• Pikipiki (Honda XL125, Yamaha 125G na Suzuki 125CC)<br>• Vifaa vingine | 20 hadi 22 Februari, 2026 |
| 4. | Arusha | Benki Kuu ya Tanzania, Barabara ya Makongoro, S.L.P 3043, Arusha. | • Samani za ofisi<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa vya tehama<br>• Vifaa vining | 21 Februari, 2026 |



16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: info@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501

| Na. | Mkoa | Kituo | Kifaa | Tarehe ya Mnada |
|---|---|---|---|---|
| 5. | Mwanza | Chuo cha Benki Kuu ya Tanzania, Mtaa wa Capri-Point, S.L.P 131, Mwanza. | • Samani za ofisi<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa vya tehama<br>• Vifaa vingine | 21 Februari, 2026 |
| 6. | Mjini Magharibi (Unguja) | Benki Kuu ya Tanzania, Eneo la Gulioni, S.L.P 568, Zanzibar. | • Samani za ofisi<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa vya tehama<br>• Vifaa vingine | 25 Februari, 2026 |
| 7. | Dodoma | Benki Kuu ya Tanzania, Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete 40184, S.L.P 2303, Dodoma. | • Samani za ofisi<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa vya tehama<br>• Vifaa vingine | 26 Februari, 2026 |
| 8. | Mwanza (Tawi) | Benki Kuu ya Tanzania, Barabara ya Makongoro, S.L.P 1362, Mwanza. | • Samani za ofisi<br>• Vifaa vya ofisi<br>• Vifaa vya tehama<br>• Vifaa vingine | 28 Februari, 2026 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo.
2. Malipo ya vifaa chakavu ni asilimia mia moja (100%) na mteja atatakiwa kuondosha vifaa chakavu alivyonunua siku ya mnada.
3. Mnunuzi wa gari, pikipiki na mitambo atalazimika kulipa papo hapo amana “deposit” isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya bei na atatakiwa kukamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Mnunuzi wa gari, pikipiki na mtambo atatakiwa kuondoa/kuchukua mali aliyonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Gharama za kubadilisha umiliki (magari, pikipiki na mitambo) ni jukumu la mnunuzi na anatakiwa kukamilisha taratibu za kumilikishwa chombo kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
6. Ruhusa ya kuangalia vifaa itatolewa siku mbili (2) kabla ya mnada husika kuanzia saa nne (4:00) asubuhi hadi saa kumi jioni (10:00).
7. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi katika vituo vilivyoorodheshwa hapo juu.

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**



16 Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P. 2303, 40184 Dodoma - Tanzania,
Barua Pepe: info@bot.go.tz, Tovuti: www.bot.go.tz, Simu: +255 22 223 2541/2501